



## Masomo ya watoto wakubwa wa CBM

### Somo la 2 Mungu anaumba dunia

#### SOMA Mwanzo 1 na 2

##### SOMO

Mungu ni muumba. Nguvu za mwenyezi Mungu ndizo zilitengeneza dunia na vyote vilivymo. Mungu ni Muumba wa mbingu na nchi.

**Hapo mwanzo:** Mstari wa kwanza wa Biblia unasema, "Hapo mwanzo Mungu alizumba mbingu na nchi." Haya yote yalifanyika miaka mingi sana iliyopita. Hatujui hii ilifanyika lini au ilichukua miaka mingapi kutengeneza mbingu na nchi. Wakati huo dunia ilikuwa giza, ukiwa na ilifunika kwa maji.

**Siku sita za uumbaji:** Baadaye, Mungu aliamua kuumba dunia tunamoishi. Mungu alikuwa na mpango wa kuumba mwanadamu lakini alitaka aishi mahali pazuri. Hii ilionyesha vile Mungu alimpenda. Siku ya kwanza ya kuumba Mungu alisema, "Na kuwe na nuru." Mungu akafanya nuru. Kukawa na nuru na giza. Kukawa mchana na usiku.

Kwa siku sita Mungu akaumba dunia hii.

Kwa kila siku aliumba:

Siku ya 1 – Nuru

Siku ya 2 – Gawanyisha bahari na mawingu.

Siku ya 3 – Nchi na mimea

Siku ya 4 – Jua, mwezi na nyota

Siku ya 5 – Samaki na ndege

Siku ya 6 – Wanyama na mtu



**Roho ya Mungu** Mungu aliumba dunia yetu kwa siku sita. Kwa kila siku Mungu aliamrisha. Tunasoma Mungu akisema, "Na kuwe na ...." Nakila siku kuliumbwa alichoamrisha Mungu. Mungu aliona vyote vilikuwa vizuri. Kila kitu kiliumbwa kwa maneno aliyojasema.

#### Maswali na Majibu

1. Dunia ilikuwa namna gani hapo awali?

*Ilikuwa giza, tupu, ilifunika kwa maji na nafsi ya Mungu ilitanda juu ya maji.*

2. Kwa hizo siku 6, Mungu alitengeneza nini kwa kila siku?

*1 nuru; 2 mawingu/anga/bahari; 3 nchi na mimea; 4 jua, mwezi na nyota 5 samaki na ndege; 6 wanyama na mtu*

3. Mungu alifanya nini siku ya 7? Na sisi tufanye nini?

*Mungu alistarehe; hata nasi tusitarehe na tutumie hiyo siku kuabudu Mungu.*

4. Nafsi wa Mungu ni nini?

*Ni neno lake au pumzi yake, na ndiyo nguvu zake.*

5. Tukiona viumbe vyta Mungu tunatakiwa tufanye nini?

*Tunatakiwa tumwamini, tumpende Mungu kwa sababu ameonyesha vile anatupenda.*

6. Mungu alitengeneza mtu namna gani?

*Alitengeneza tu mfano, kutoka kwa mavumbi, akapuliza pumzi ya uzima ndani ya mapua yake.*

7. Nafsi ni nini? *Uhai*

8. Mungu alipea Adamu kufanya kazi gani? *Kutunza bustani na wanyama*

9. Mungu alitengeneza mwanamke namna gani?

*Alifanya Adamu akalala usingizi mzito na akatoa ubavu na kutengeneza mwanamke.*

10. Hii inatufunza nini juu ya ndoa?

*Shirikiana, mume mmoja, mke mmoja maisha yote, oa na utoke nyumbani.*

**Mistari ya kukariri** Mwanzo 2:7; Mathayo 19:4 – 6


#### Mazungumzo Nafsi inaweza kuishi milele?

Soma mistari zifuatazo kutoka kwa Biblia. Soma na mpate maana yake halafu mtapata jibu la swali. *Mwanzo 2:7; 1 Timotheo 6:15 – 16; Zaburi 89:48; Muhubiri 9:5 – 6; Ezekiel 18:4*

#### Kuandika

Mungu alitengeneza mwanamke namna gani na kwa nini? Tunajifunza nini kuhusu ushirikiano wa mume na mke? (Mathayo 19:4 – 6).

Zaburi 33 mstari wa 6 unasema, "Kwa meno la Bwana mbingu zilifanyika, na jeshi lake lote kwa pumzi ya kinywa chake." Hii inatwambia kwamba kila kitu kiliumbwaa 'kwa meno la Bwana.' Mungu alisema na ilifanyika. Mstari unaofwata unarudia hayo hayo tu ukisema nyota zilitengenezwa kwa pumzi ya kinywa cha Mungu. Tukinena tunatumia pumzi ya kinywa chetu, kwa hivyo hii inamaanisha kwamba meno la Mungu liliumba dunia. Neno la Mungu ni pumzi ya Mungu. Nafsi ni pumzi, kwa hivyo meno la Mungu wakati mwiningine inaitwa nafsi wake. Neno la Mungu au pumzi au nafsi ni uwezo wake. Ni uwezo ndiyo Mungu alitumia kuumba dunia yote. Mungu anatumia uwezo wake kufanya kila kitu.



Kila kitu duniani kinachotizingira chaonyesha kwamba Mungu aki. Kila mtu huona vyote vilivyoumbwa na Mungu hapa duniani lakini wanakataa kumwabudu. Tukiangalia vyote vilivyo karibu na sisi tunashangaa vile ni vizuri na vile kila kitu kinafanya kazi. Ni kawaida na tunaamini viliundwa na muumba mkuu.

Tunatakiwa tukubali na tuamini kwamba Mungu ndiye muumba. Tuamini Mungu na tujue kwamba Mungu anapenda mwanadamu na anataka aishi kwa hii dunia nzuri. Tunaabudu Mungu wa ajabu na ni wa upendo.

Warumi 1:20 – 21 "Kwa sababu mambo yake yasiyoonekana tangu kuumba ulimwengu yanaonekana na kufahamika kwa kazi zake; yaani, uwezo wake wa milele na Uungu wake, hata wasiwe na vijisababu. Kwa sababu walipomjua Mungu, hawakumtukuza kama ndiye Mungu wala hawakumshukuru; bali walipotea katika uzushi wao, na mioyo yao yenye ujinga ikatiwa giza."

**Mungu anafanya mtu:** Mungu alifanya mtu siku ya sita: siku hiyo ndiyo alifanya wanyama. Mungu aliumba mtu kutoka kwa mchanga. Mungu alichukua vumbi au mchanga na kutengeneza mfano wa mtu. Halafu Mungu akapuliza pumzi ndani ya mapua ya mtu na mtu akawa hai. Mungu alipopuliza pumzi ndani ya mapua, mtu akaishi au akawa nafsi hai.

Mungu alimfanya Adamu kuwa mtawala wa wanyama na akawapa mimea na miti kuwa vyakula vyao. Mungu alitengenezea bustani ya ajabu ili aishi ndani. Kazi yake ilikuwa kuitunza hiyo bustani.

Mungu alimfanya mtu na akili ya kufikiri na kuamua. Mtu anaweza kujifunza juu ya Mungu na kumpenda. Adamu aliona wanyama wote na akawapa majina. Lakini hakukuwa na mnyama aliyefaa kuwa mwenzi wa Adamu. Hawakuweza kuzungumza naye wala kushiriki maisha. Hawangeweza kujifunza juu ya Mungu na wasaidie Adamu kupenda Mungu na kumtii.

**Mungu anatengeneza mke:** Mungu alifanya Adamu akalala usingizi mzito. Akatwaa ubavu moja kutoka kwa Adamu na akamtengezea mwenzi wake. Adamu akamuita 'mwanamke' maana yake 'ametwaliwa kutoka kwa mume'.



Mwanamme analistahili kuwa na mwenzi wake aliye msaidizi. Mungu alijua na akaletea Adamu mke. Mungu ametupa ndoa ili tupate mtu wa kusaidiana naye. Mungu alitengeneza mume mmoja na mke mmoja ili wawe wamoja. Hili somo ni kwamba Mungu alitengeneza mume mmoja na mke mmoja wawe hivyo kwa maisha yote. Mungu aliashiria mume na mke wafanye kazi pamoja tena wasadiane.

Yesu alisema kwamba hii mistari kutoka kwa kitabu cha Mwanzo inatufundisha juu ya ndoa. Mume akioa, yeche na mkewe wanatakiwa watoke kwa nyumba ya wazazi wao na wawe kwa boma lao. Waanzishe familia yao na lazima wafanye kazi pamoja kwa maisha yao yote na wawe waaminifu mmoja kwa mwenzake. Njia nzuri ya kuishi vizuri ni kumsaidia mwenzako ampende na kumtii Mungu.

Chagua mwenzio wa ndoa kwa umakini sana. Anatakiwa awe mwenzi mzuri kwa maisha yako yote. Mtashirikiana kwa furaha, kwa shida, kwa uchungu, kwa mambo yote mpaka ukufe. Anatakiwa awe mtu atakaye kusaidia kujua na kupenda Mungu.

**Siku ya saba:** Baada ya siku sita Mungu alikuwa amemaliza kuumba ulimwengu na kila kitu kilichomo. Mungu aliangalia kila kitu alichotengeneza na akaona ni kizuri sana. Siku ya saba, Mungu alistarehe. Hata na sisi tunatakiwa tupumzike siku moja kwa wiki. Siku yetu ya kustarehe ni Jumapili ingawaje haijalishi siku ya kustarehe. Tunatumia siku ya kustarehe kuabudu Mungu. Lakini tunapashwa kupenda Mungu na tumtii kila siku.